# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.9 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) NOVEMBA 2021

# WANAOBAMBIKIZIA KESI WALIMU WAONYWA



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba*



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde akitoa hotuba ya ufunguzi wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutoka Wilaya 139 za Tanzania Bara. Kikao hicho kilifanyika Oktoba 21-22, 2021 jijini Dodoma.*

**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

# TUSISAHAU KUBORESHA MAZINGIRA YA KAZI YA WALIMU

Hivi karibuni Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitangaza kupatikana kwa fedha za jumla ya shilingi trilioni 1.3 na kutoa mgawanyo wa matumizi ya fedha hizo katika kuboresha miundombinu mbalimbali katika Sekta ya Afya na Elimu ikiwa ni kuunga mkono juhudi za dunia nzima katika mapambano dhidi ya virusi vya Corona vinavyosababisha ugonjwa wa homa kali ya mapafu (UVIKO-19).

Hatua hii kwa njia moja au nyingine itasaidia kuboresha miundombinu ya elimu yakiwemo madarasa, ofisi za walimu, samani, nyumba za walimu, n.k vitakavyosaidia katika kuboresha elimu nchini kwa kupunguza au kondoa kabisa ujinga na umaskini na kusaidia kukuza uchumi wa Taifa.

Tunawapongeza sana wadau wa maendeleo hapa nchini ambao pamoja na mambo mengine ya maendeleo ya Taifa, wamebaini nasi tunawajibika kubaini kuwa Elimu sio njia ya kuepukana na umaskini, bali ni njia ya kupambana nao. Hali kadhalika walimu ndiyo nguzo muhimu katika kukuza uelewa, na ukitaka Taifa bora, basi boresha elimu, na ukitaka kuboresha elimu, basi boresha walimu. Hii inahitimisha kwamba ukitaka Taifa la watu wanaojiheshimu, heshimu walimu.

Heshima ya walimu inaletwa na mambo mengi mojawapo likiwa ni kuwa na mazingira bora ya kazi, makazi, na stahiki muhimu kwa walimu kwa mujibu wa Sheria na taratibu za ajira zao.

Hivyo, ni imani yetu kuwa fedha hizo zitatumika vizuri katika kufikia malengo yaliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya utendaji kazi ya walimu ili waeendelee kuwafundisha wanafunzi kwa bidii, weledi na uzalendo.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama


**Wajumbe**
Moses Chitama
Christina Hape
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***
*Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania* *tumeyautumishiwawalimutanzania*

# WANAOBAMBIKIZIA KESI WALIMU WAONYWA



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde akitoa hotuba ya ufunguzi wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutoka Wilaya 139 za Tanzania Bara. Kikao hicho kilifanyika Oktoba 21-22, 2021 jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba akitoa neno la kumkaribisha Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde ili afungue Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka wilaya 139 za Tanzania Bara kilichafanyika Oktoba 21-22, 2021 jijini Dodoma.*



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka Wilaya 139 za Tanzania Bara kilichafanyika Oktoba 21-22, 2021 jijini Dodoma.*

**Na Mwandishi wetu.**

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imewataka Kaimu Katibu Wasaidizi 139 Wilayani wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), kuacha kuwabambikizia makosa walimu ili wasionekanane watendaji wazuri jambo linalopelekea kutopandishwa kwao madaraja.

Aidha imepiga marufuku kuomba au kuweka mazingira ya rushwa kwa walimu ili waweze kuwapendekeza majina yao katika upandishwaji madaraja.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI Mhe. David Sulinde, wakatia kifungua Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa Tume kutoka wilaya 139 kilichofanyika jijini Dodoma.

Mheshimiwa Silinde alisema hataki kusikia walimu wanabambikiwa makosa na Makatibu hao na endapo atabaini hilo hatua kali dhidi yao zitachukuliwa.

"Sitaki kusikia suala la kumbambikizia makosa walimu. Hiyo inachangia

kumkosesha mwalimu nafasi ya kupandishwa daraja,"alisema Silinde.

Hata hivyo alisema hakuna sababu ya kuweka bifu na walimu na kupelekea kuwabambikizia makosa jambo ambalo wanajenga uadui baina yao na kushusha morali ya utendaji kazi katika maeneo yao.

Mbali na hilo alisema anapiga vita suala la rushwa wanalodaiwa walimu ili waweze kupandishwa daraja katika ngazi walizokuwa nazo mashuleni kwani Katibu Wasaidizi wanatakiwa kutenda haki na sio kuingia katika ubadhirifu, uvunjaji Sheria, na uonevu.

Alisema TAMISEMI ikibaini kuna Katibu Msaidizi anayefanya hivyo basi hatua kali zitachukuliwa dhidi yake kwani Serikali inawaamini sana kutokana na utendaji kazi wao.

"Nawapongeza sana kwenye suala la kupandisha walimu madaraja, lakini nasisitiza kuwa rushwa iachwe kwani walimu wenye sifa wanapaswa kupewa nafasi ya kupandishwa madaraja,"alisema Silinde.

Alisema rushwa ni adui wa haki na haipaswi kuingizwa kazini hivyo ni vema wakaliacha na

# WANAOBAMBIKIZIA KESI WALIMU WAONYWA



*Badhi ya washiriki wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka Wilaya 139 za Tanzania Bara kilichafanyika wakiwa katika hali ya utulivu wakati kikao hicho kinaendelea.*

kuwapa nafasi walimu ya kufanya kazi kwa bidi bila makandokando yoyote.

Akizungumzia suala la fedha zilizotolewa na Mheshimiwa Rais alisema jumla ya shilingi billioni 536.6 ambazo zilitolewa TAMISEMI na shilingi billioni 304 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya elimu hivyo kusisitiza ziende zikatumike ipasavyo katika miradi hiyo.

Mbali na hilo alizitaka halmashauri kuhakikisha zinawapatia mara moja Kaimu



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kulia), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) pamoja na Wajumbe wa Menejimenti ya TSC wakati wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka wilaya 139 za Tanzania Bara kilichafanyika Oktoba 21-22, 2021 jijini Dodoma.*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kulia), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) baadhi ya Kaimu Katibu Wasaidizi walioshiriki Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka wilaya 139 za Tanzania Bara kilichafanyika Oktoba 21-22, 2021 jijini Dodoma.*

# WANAOBAMBIKIZIA KESI WALIMU WAONYWA



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde (katikati) akitoka kwenye ukumbi wa Chuo cha Mipango, Dodoma mara baada ya kufungua Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kilichofanyika Oktoba 21-22, 2021 jijini Dodoma. Upande wa Kushoto ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama na upande wa kulia ni Mkurugenzi wa Elimu kutoka TAMISEMI, Ephraim Simbeye.*

Katibu Wasaidizi Wilaya ofisi zenye hadhi ya kufanyia kazi na sio kuwaacha wakifanya kazi katika mazingira ambayo hayastahili na atakayekwenda kinyume na maelekezo hayo Wizara itachukua hatua kwa namna ambavyo itaona inafaa.

Ukiacha hilo alisema ofisi yake inaliangalia suala la bajeti kwa jicho la pekee ili kuhakikisha wanafanya kazi katika mazingira yenye weledi ambayo yataifanya Tume na walimu kwa ujumla wao kufanya kazi kwa weledi mkubwa na kuleta mafanikio tarajiwa nchini.

Silinde alitoa wito kwa walimu kushiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya elimu hapa nchini.

Kwa upande wake Katibu wa TSC Mwl. Paulina Nkwama, alisema Tume hiyo itahakikisha fedha zilizotolewa zitatumika ipaswavyo katika miradi ambayo inatekelezwa hapa nchini.

Alisema wanaihakikishia OR-TAMISEMI kila kitu kilichopangwa kitakwendaCipasavyo ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati.

"Tumejipanga kuhakikisha tunatekeleza kile tulichoagizwa hivyo msiwe na wasiwasi na Tume," alisema Nkwama.

Naye Mwenyekiti wa TSC Profesa Willy Komba alisema vitendo vya uonevu havitakuwa na nafasi katika Tume hiyo, hivyo watahakikisha kila mmoja anafanya kazi yake bila ya kuonewa na mtu.

Alisema Tume hiyo inasimamia haki hivyo suala la rushwa halipewi nafasi kwenye utendaji wa Tume wa kila siku.



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Christina Hape akisalimia wajumbe waliohudhuria Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka wilaya 139 za Tanzania Bara.*

# MAKAMU WA RAIS AFUNGUA MASHINDANO YA SHIMIWI



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango akikabidhi Mpira wa mikono kwa mwakilishi wa timu za mpira wa mikono wakati wa ufunguzi wa Michezo ya 35 ya SHIMIWI inayofanyika katika uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.*




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (mwenye miwani na suruali nyeupe) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC wanaoshiriki mashindano ya SHIMIWI mkoani Morogoro.*

**Na Mwandishi Wetu**

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango, Oktoba 23, 2021 amefungua Michezo ya 35 ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) inayofanyika katika viwanja mbalimbali mkoani Morogoro ambapo Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ni miongongi mwa washiriki wa mashindano hayo.

Akifungua Michezo hiyo, Dkt. ameagiza Watendaji Wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kuhakikisha wanatenga muda kwaajili ya watumishi wa serikali kufanya mazoezi walau siku moja katika wiki huku akiwataka watendaji wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ambazo hazijashiriki katika mashindano hayo kwa mwaka 2021 kujieleza kwa maandishi kwa Waziri Mkuu sababu za kutoshiriki mashindano hayo.

Vilevile, Makamu wa Rais ameagiza ofisi zote za Serikali zinazopaswa kushiriki mashindano hayo kuhakikisha bajeti za ushiriki katika michezo zinapangwa mapema, na kuruhusu watumishi kufanya mazoezi kwa muda muafaka ili kuongeza ushindani katika mashindano hayo.

Aidha Makamu wa Rais amekemea vikali ushiriki wa wanamichezo wasiowatumishi wa Umma katika Mashindano hayo huku akiitaka Wizara ya Sanaa Michezo na Utamaduni kwa kushirikiana na Uongozi wa

# MAKAMU WA RAIS AFUNGUA MASHINDANO YA SHIMIWI




*Watumishi wa TSC wakiwa na bango wakati wa maandamano ya kuelekea ufunguzi wa mashindano ya SHIMIWI kwa mwaka 2021 mkoani Morogoro.*

SHIMIWI, kujiridhisha kwa kina kwamba katika mashindano hayo washiriki wote ni watumishi wa Umma na endapo itabainika kuwepo kwa wachezaji wasio watumishi wa Umma hatua kali zichukuliwe.

Katika hatua nyingine Makamu wa Rais ametoa wito kwa wananchi wote kuendelea kushiriki katika michezo pamoja na kufanya mazoezi ili kupunguza hatari ya kupata magonjwa yasioambukiza. Amesema katika taarifa ya hali ya Magonjwa yasiyoambukiza na Umaskini hapa nchini iliyotolewa mwaka 2020 na Kamisheni ya Magonjwa Yasiyoambukiza, inaonyesha kuwa, magonjwa hayo yanachangia zaidi ya asilimia 33 ya vifo vyote nchini hivyo watanzania hawana budi kuwekeza muda katika kushiriki michezo pamoja na mazoezi.

Pia Makamu wa Rais amemuagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo kuanza mapema mchakato wa kuwashirikisha watumishi wa umma wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili mwakani waweze kushiriki Michezo ya Shimiwi.

Tume ya Utumishi wa walimu nayo imepeleka watumishi wake katika mashindano hayo ambapo wanashiriki michezo ya kuvuta kamba, mpira wa pete, mpira wa miguu, karata, bao, *draft*, kuendesha baiskeli pamoja na riadha.



*Watumishi wa TSC wakiwa katika maandamano ya kuelekea ufunguzi wa mashindano ya SHIMIWI kwa mwaka 2021 mkoani Morogoro.*




*Watumishi wa TSC wakiwa katika maandamano ya kuelekea ufunguzi wa mashindano ya SHIMIWI kwa mwaka 2021 mkoani Morogoro.*

# MAKAMU WA RAIS AFUNGUA MASHINDANO YA SHIMIWI



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (upande wa kulia mwenye miwani) akiwa katika picha ya pamoja na wachezaji wa mpira wa pete wa TSC wakati wa mashindano ya SHIMIWI mkoani Morogoro.*



*Watumishi wa TSC wakishangilia wakati wa mashindano ya SHIMIWI yanayofanyika mkoani Morogoro.*




*Wachezaji wa mpira wa pete wa TSC (rangi ya bluu) wakicheza kwenye mashindano ya SHIMIWI*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (kulia) akiwa katika mazungumzo na Mwenyekiti Mstaafu wa TSC, Oliva Mhaiki wakati mwenyekiti huyo mstaafu alipotembelea ofisi za TSC hivi karibuni.*



*Picha ikionesha baadhi ya wajumbe wa Kamati ya TEHAMA ya TSC wakiwa wanaendelea na kikao cha kamati hiyo kilichofanyika mapema mwezi Oktoba 2021 katika ukumbi wa mikutano wa TSC Makao Makuu, Dodoma.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (kushoto) akiwa katika mazungumzo na Mwenyekiti Mstaafu wa Tume, Oliva Mhaiki (kulia) pamoja na Wakurugenzi wengine wa Tume hiyo wakati mwenyekiti huyo mstaafu alipotembelea ofisi za TSC hivi karibuni.*



*Picha ikionesha baadhi ya wajumbe wa Kamati ya TEHAMA ya TSC wakiwa wanaendelea na kikao cha kamati hiyo kilichofanyika mapema mwezi Oktoba 2021 katika ukumbi wa mikutano wa TSC Makao Makuu, Dodoma.*



*Picha ikionesha wajumbe wa Kamati ya TEHAMA ya TSC wakiwa wanaendelea na kikao cha kamati hiyo kilichofanyika mapema mwezi Oktoba 2021 katika ukumbi wa mikutano wa TSC Makao Makuu, Dodoma.*



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akiongoza kikao cha Kamati ya TEHAMA kilichofanyika mapema Mwezi Oktoba 2021, katika ukumbi wa mikutano wa TSC Makao Makuu, Dodoma. Pembeni yake ni Katibu wa Kamati hiyo, Kainda Ndasa.*

# TSC YAWANOA WATUMISHI WAKE WANAOCHAMBUA RUFAA

**Na Mwandishi Wetu**

Tume ya utumishi wa walimu (TSC) imeendesha mafunzo kwa watumishi wake wa Makao Makuu ambao wanaohusika na uchambuzi wa rufaa zianzokatwa Tume Makao Makuu kupinga uamuzi wa mashauri yanayotolewa uamuzi na TSC ngazi ya Wilaya.

Akifungua mafunzo hayo yaliyofanyika Oktoba 4-6, 2021 katika Ukumbi wa Kumbukumbu na Nyaraka jijini Dodoma, Katibu wa Tume hiyo, Paulina Nkwama alisema kuwa mafunzo hayo ni muhimu kwani yanalenga kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kuisaidia Tume kutenda haki katika kuamua rufaa zinazowasilishwa mbele yake.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo yanakusudia kuwawezesha watumishi wa Tume ya Utumishi wa walimu kuondoa kabisa au kupunguza changamoto zinazojitokeza wakati wa kuchambua Rufaa kwa kuainisha upungufu kuanzia eneo la kupokea, kusajili na kuchambua rufaa.

"Katika uchambuzi, mafunzo haya yatapanua uelewa wenu katika maeneo ya Mashtaka, Uchunguzi na Uamuzi, kuangalia iwapo taratibu zimezingatiwa na ukweli kuhusu tuhuma na ushahidi. Aidha, mtaelekezwa kuchambua maeneo yote kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo," alisema Nkwama.

Aliongeza kuwa matarajio ya Serikali ni kuona Tume inatatua changamoto za walimu zinazohusu ajira, maadili na maendeleo ya walimu, kwani ndiyo msingi wa kuanzishwa kwa chombo hicho.

"Napenda kukumbusha kwamba Tume ya Utumishi wa Walimu ni chombo kinachosimamia uzingatiaji wa maadili ya kazi ya Ualimu. Hivyo, tuna wajibu wa kutoa elimu kwa walimu ili kuimarisha nidhamu katika Utumishi wa Umma na hivyo, kuchochea kasi ya maendeleo kwa Taifa letu," alisema Katibu huyo.

Nkwama alihitimisha kwa kusema kuwa, "ninaamini kuwa, baada ya mafunzo haya, tutaweza kuboresha uchambuzi wetu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo. Aidha, tutatenda wajibu wetu kwa uaminifu bila kunyima haki kwa Warufani na kuishauri Kamati ya Rufaa na Tume kwa ujumla kwa hekima na weledi wa hali ya juu."



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama*

# TSC Nzega kutoa Elimu uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali TSC, Gerard Chami (kushoto) akiongea na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Nzega, Leonard Japhet juu ya masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu katika wilaya hiyo.*

**Na Mwandishi Wetu**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nzega inaendelea na mikakati ya kuwaelimisha wadau mbalimbali juu majukumu ya Tume hiyo katika kusimamia Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu ya mwaka 2015 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2016 ili kuondoa mitazamo hasi kwa baadhi ya wadau pale TSC inapoamua mashauri ya nidhamu ya walimu.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Nzega, Leonard Japhet wakati akizungumza na Jarida la Sauti ya TSC hivi karibuni ambapo aliweka bayana kuwa wakati mwingine waajiri wanaitazama mamlaka ya nidhamu (TSC) kwa jicho hasi pale inapotokea Tume hiyo inatoa uamuzi wa shauri la nidhamu la mwalimu ambao unakwenda kinyume na matarajioa yao.

Alifafanua kuwa baadhi ya waajiri wanategemea kuwa wakimshitaki mwalimu kwenye mamlaka ya nidhamu, ni lazima aadhibiwe bila kujua kwamba mchakato wa kuendesha shauri la nidhamu hadi kufikia uamuzi una taratibu zake ambazo haziegemei upande wa mwajiri wala wa mwalimu.

"Mkurugenzi anapomshtaki mwalimu anatarajia kuwa ni lazima sisi tumfukuze kazi. Lakini sisi ni chombo huru ambacho hakipaswi kushinikizwa na mtu yeyote katika kutoa uamuzi. Sasa pale tunapofikia uamuzi wa kumwachia mwalimu kwa kuwa hakuna uthibitisho wa tuhuma, wakurugenzi wanachukia na hapo tunaanza kupishana," alisema Japhet.


Alieleza kuwa kutokana na changamoto hizo, wanakusudia kukaa na waajiri pamoja na wadau wengine wa elimu ili kwa pamoja waweze kuelimishana juu ya namna TSC inavyofanya kazi zake kwa kuzingatia haki za pande zote mbili.

Kwa mujibu wa kaimu Katibu Msaidizi huyo, katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Septemba 2021 jumla ya mashauri ya nidahamu 20 yalianzishwa



*Mtumishi wa TSC Nzega, Andrew Mabala akiwa anaendelea kutekeleza majukumu yake ya kila siku ofisini kwake.*

# TSC Nzega kutoa Elimu uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu



*Mtumishi wa TSC Nzega, Alice Nshunju akiwa anaendelea kutekeleza majukumu yake ya kila siku ofisini kwake.*

ambapo makosa ya utoro kazini ndiyo yaliyochukua nafasi kubwa yakifuatiwa makosa ya ulevi.

Katika idadi hiyo ya mashauri yaliyofunguliwa, 17 yalihitimishwa ambapo walimu watatu waliachiwa huru baada ya kutopatikana na hatia huku wengine wakipewa adhabu mbalimbali ikiwemo kufukuzwa kazi, kushushwa cheo na onyo baada ya kukutwa na hatia katika tuhuma zilizokuwa zinawakabili.

Kama ilivyo katika wilaya nyingine, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Nzega anaeleza kuwa moja ya changamoto inayowakabili walimu katika wilaya hiyo ni utoro ambapo baadhi yao hasa vijana wanatoroka kwa lengo la kutafuta kazi zinazowapatia kipato kikubwa kwa haraka.

Hata hivyo, kiongozi huyo alieleza kuwa baadhi ya walimu hao wanatoroka bila kufanya utafiti juu ya kile wanachowenda kukifanya kitu ambacho kinawafanya baada ya muda mfupi kurudi wakiomba warudishwe kazini kutokana na maisha kuwa magumu zaidi.

"Yaani unakuta mwalimu amejazwa maneno, anaamua kuacha kazi na kujiingiza kwenye biashara nyingine akidhani huko kuna maslahi makubwa. Tunajaribu kuwashauri lakini hawaelewi kabisa, sasa baada ya muda mfupi kile alichokuwa anatarajia kupata hakioni anaanza kujuta na kuomba arudishwe kazini lakini wakati huo anakuwa amechelewa," alisema.

Ofisi ya TSC Nzega inahudumia Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Mji Nzega na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ambapo halmashauri ya mji ina shule za msingi 31 na 11 za sekondari zinazomilikwa na Serikali huku ikiwa na walimu 444 wa shule za msingi na 148 wa sekondari.

Kwa Upande wa Halmashauri ya Wilaya kuna jumla ya shule za serikali 180 ambapo katika idadi hiyo shule 149 ni za msingi na shule 31 ni za sekondari na jumla ya walimu 1547 ni wa shule za msingi na 450 ni wa sekondari.



*Mtumishi wa TSC Nzega, Florah Paschal akiwa anaendelea kutekeleza majukumu yake ya kila siku ofisini kwake.*

# TSC Nzega kutoa Elimu uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu






*Mtumishi wa TSC Nzega, Catherine Shija akiwa ofisni kwake.*



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Nzega wakiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali TSC, Gerard Chami (wa tatu kutoka kushoto) wakati Mkuu huyo wa Kitengo alipotembelea ofisi ya TSC Nzega hivi karibuni.*

# TSC MPWAPWA YAENDESHA MAFUNZO KWA WALIMU WA AJIRA MPYA

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mpwapwa imeendesha mafunzo elekezi yaliyolenga kuwajengea uwezo walimu wa ajira mpya ya Julai 2021 juu ya sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa walimu.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mpwapwa, Patricia Binde akiwasilisha mada kuhusu Miiko na Maadili ya Kazi ya Ualimu kwenye Mafunzo Elekezi yaliyotelewa na TSC kwa walimu wa ajira mpya ya Julai 2021. Mafunzo hayo yalifanyika hivi karibuni wilayani Mpwapwa.*



*Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Noel Abel akikabidhi kielelezo cha Nguzo Kuu za Kazi ya Ualimu pamoja na Mikataba ya Ajira kwa Walimu wa ajira mpya ya Julai 2021 wakati wa Mafunzo Elekezi kwa watumishi hao.*



*Afisa Maadili wa TSC Wilaya ya Mpwapwa, Appolo Musa akitoa maelekezo kwa Walimu wapya Ajira ya Julai 2021 waliohudhuria Mafunzo Elekezi yaliyofanyika hivi karibuni wilayani Mpwapwa.*



*Afisa Maadili na Nidhamu wa TSC Mpwapwa, Noel Lukupe akiwasilisha Mada kuhusu Nguzo kuu za maadili ya Kazi ya Ualimu Kwa Walimu wapya ajira ya Julai 2021 katika Mafunzo Elekezi yaliyofanyika hivi karibuni Wilayani Mpwapwa.*



*Kaimu Mthibiti Ubora wa Shule Wilaya Mpwapwa, Hilary Edwin akiwasilisha Mada kuhusu Mbinu za ufundishaji na Utekelezaji wa Mtaala wa Elimu kwenye Mafunzo Elekezi Kwa Walimu wapya Ajira ya Julai 2021 yaliyofanyika hivi karibuni wilayani Mpwapwa.*



*Afisa Ajira wa TSC Wilaya ya Mpwapwa, Angela Bureta akiwasilisha Mada kuhusu Masala mbalimbali ya Ajira na Maendeleo ya Walimu kwenye Mafunzo Elekezi Kwa Walimu wapya wa Ajira ya Julai 2021 waliopangiwa vituo vya kazi katika shule za Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.*

# Walimu Nyamhongolo wahimizwa kujiendeleza katika taaluma zao

**Na Mwandishi Wetu**

Walimu wa shule ya MsingiNyamhongolo iliyopo Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza wamehimizwa kujiendeleza kielimu katika kitaaluma zao ili pale wanapomaliza waweze kubadilishiwa cheo/kazi kwa mujibu wa taratibu za utumishi wa walimu bila kupata usumbufu.

Kauli hiyo imetolewa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya



*Walimu wa Shule ya Msingi Nyamhongolo wakiwa wanaendelea kutekeleza majukumu yao.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ilemela Fundikira James akiongea na walimu wa Shule ya Msingi Nyamhongolo (hawapo pichani) wakati wa ziara yake katika shule hiyo aliyoifanya hivi karibuni. Upande wa kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gererd Chami na kushoto ni Mkuu wa Shule hiyo, Mwl. Basadi Lugiko.*



*Mmoja wa walimu wa Shule ya Msingi Nyamhongolo akiwa anafunsisha darasani.*



*Walimu wa Shule ya Msingi Nyamhongolo wakiwa katika Picha ya pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gererd Chami (aliyevaa koti, mwenye miwani) pamoja Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ilemela Fundikira James (aliyevaa suti) wakati viongozi hao walipotembelea shule hiyo hivi karibuni.*

# Walimu Nyamhongolo wahimizwa kujiendeleza katika taaluma zao

ya Ilemela, Fundikira James wakati wa ziara yake aliyoifanya shuleni hapo hivi karibuni kwa lengo la kuwakumbusha walimu hao taratibu mbalimbali za utumishi wa walimu.

"Wengi wetu tunajiendeleza ili tuweze kufanyiwa recategorization (kubadilishiwa kazi/cheo) ndani ya kada ya ualimu. Sasa ni lazima tujue kwamba ili uweze kufanyiwa hivyo ni lazima ujiendeleze katika katika ualimu, ukienda nje ya kada ya ualimu ujue kwamba sisi tatuna mamlaka ya kukubadilishia kazi," alifafanua.

Aliendelea kusema kuwa, "baadhi ya walimu wamekuwa wakilalamika kuwa wamesoma lakini hawabadilishiwi cheo, unapokuja kuangalia vyeti vyao unakuta wamejiendeleza nje ya taaluma zao. Wakati mwingine hii inatokea kwa sababu ya kukosa ushauri na mwongozo sahihi kabla ya kwenda masomoni."

Fundikira aliendelea kueleza kuwa kutokana na changamoto hizo TSC imekuwa ikikutana na walimu na kuwaeleza taratibu za kuzingatia pale wanapoamua kwenda masomoni ili kila mmoja anapojiendeleza ajue faida atakazozipata katika taaluma yake.

"Kabla hujaamua kwenda masomoni tafuta ushauri kwa viongozi wako ili ujue kile unachotaka kukisomea kitakufikisha katika malengo unayokusudia au la. Usiende tu kusoma kwa kuwa una fedha za kujisomesha, ofisi yangu ipo wazi muda wote kwa ajili ya kuwasidia katika masuala yote yanayohusu utumishi wenu," alisema Fundikira.

Pamoja na kuwahimiza kujiendeleza, Kaimu katibu Msaidizi huyo aliwataka walimu kuhakikisha wanapata ruhusu kutoka kwa mwajiri wao kabala ya kuondoka kwenye kituo cha kazi kwenda masomoni ili kuondokana na hatua za kinidhamu zinazoweza kuchukuliwa kwa kuondoka bila kufuata taratibu.

Vilevile aliwaeleza kuwa kama mwalimu ana kusudia kwenda masomoni ni lazima afanye maandalizi mapema ikiwa ni pamoja na kuhakikisha anaingizwa kwenye mpango wa mafunzo wa mwaka anaokusudia kwenda kusoma pamoja na kuwasilisha maombi ya ruhusa kwa mwajiri kabla ya muda wa kwenda masomoni haujafika.

"Kujiendeleza ni jambo zuri lakini kama lisipozingatia utaratibu unaotakiwa linaweza kukuletea shida. Kuna baadhi ya walimu wanaandika barua ya kuomba ruhusa kwenda masomoni lakini kabla hajapata kibali anaondoka, hilo ni kosa. Unapokwenda masomoni hakikisha umepata ruhusua ya mwajiri kwa maandishi, usikubali kupewa ruhusa ya mdomo, serikalini tunakwenda kwa maandishi," alisistiza Fundikira.

Pamoja na hayo, Kaimu Katibu Msaidizi huyo aliwataka walimu shuleni hapo kufanya kazi kwa bidi na kwa moyo wa uzalendo ili kuendelea kuinua kiwango cha elimu katika shule hiyo huku akiwataka kuzingatia maadili ya kazi ya ualimu wakiwa ndani na nje ya shule.





*Picha ya baadi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Nyamhongolo.*

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA YATOA HATI ZA PONGEZI KWA TIMU ILIYOFANIKISHA ZOEZI LA UPANDISHAJI NA UBADILISHAJI VYEO WATUMISHI-2021



*Afisa Utumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Getruda Gisema akitoa neno fupi wakati wa hafla ya kuipongeza timu ya watumishi waliofanikisha zoezi la kupandisha madaraja na kubadilisha vyeo watumishi wa Manispaa hiyo. Hafla hiyo imefanyika hivi karibuni katika Manispaa ya Shinyanga.*

**Na Mwandishi wetu**

Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga imetoa hati za pongezi kwa timu ya watumishi wa Halmashauri hiyo pamoja na viongozi wa vyama vya wafanyakazi na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) waliofanikisha utekelezaji wa zoezi la upandishaji vyeo na ubadilishaji vyeo watumishi wa halmashauri hiyo kwa mwaka 2021 hali iliyopelekea watumishi zaidi ya 750 kubadilishiwa mishahara kwa wakati.

Akizungumza katika hafla fupi ya utoaji hati hizo iliyofanyika hivi karibuni katika viwanja vya Mazingira Centre mjini Shinyanga, afisa utumishi wa Halmashauri ya Manispaa hiyo, Bi Getruda Gisema aliishukuru na kuipongeza timu nzima iliyohusika katika zoezi la upandishaji na ubadilishaji vyeo kwa mwaka 2021 kwa kufanya kazi hiyo kwa kujitoa na kwa weledi uliotukuka.

"Hatukulala, kuna wakati tulikuwa tunaamshana usiku wa manane kuvizia mtandao, tukawa tunakesha huku tuking'atwa na mbu lakini yote hiyo ilikuwa ni katika kufanikisha zoezi la promotion (upandishaji vyeo) ndani ya wakati kama ilivyoagizwa na serikali yetu. Nawapongezeni sana." Alisema Gisema.

Gisema aliipongeza TSC pamoja na vyama vya wafanyakazi kikiwemo Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) kwa ushirikiano



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Shinyanga, Happiness Mlangi akikabidhiwa cheti cha pongezi na Afisa Utumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Getruda Gisema.*

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA YATOA HATI ZA PONGEZI KWA TIMU ILIYOFANIKISHA ZOEZI LA UPANDISHAJI NA UBADILISHAJI VYEO WATUMISHI-2021

wao waliouonesha wakati wa zoezi hilo la upandishaji na ubadilishaji vyeo na hatimaye kufanikisha zoezi hilo ndani ya wakati na kwa ufanisi mkubwa.

Akiwataja kwa majina baadhi ya watumishi waliokuwemo katika timu hiyo, Gisema alitoa shukrani zake za pekee kwa afisa utumishi msaidizi wa Manispaa hiyo, Januari Missana kwa kazi kubwa aliyoifanya bila kuchoka usiku na mchana kwa kushirikiana na timu nzima.

"Kwa kipekee kabisa napenda kumpongeza January kwa kazi kubwa aliyoifanya usiku na mchana akishirikiana na timu nzima katika zoezi hilo. Nawapongeza pia watu wa utunzaji wa kumbukumbu (masjala) katika kufanikisha uapatikanaji wa majadala ya watumishi bila kujivutavuta. Asanteni sana." Alishukuru Gisema.

Aidha, Gisema alisema Halmashauri hiyo itaendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazo wakabili watumishi wa Halmashauri zikiwemo posho za uhamisho na malimbikizo ya mapunjo ya mishahara (salary arrears) kwa walimu.

Alisema kuwa tayari Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga amemuagiza mkaguzi wa ndani kuhakiki madeni yote ya walimu ili yaweze kushughulikiwa kwa wakati.

Awali, akizungumza katika hafla hiyo, Mwenyekiti wa Chama Cha Walimu Manispaa ya Shinyanga, Mwalimu Meshack Mashigala alisema pamoja na serikali kufanikisha zoezi la upandishaji madaraja walimu, aliiomba Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kushughulikia malalamiko ya walimu waliohamishwa vituo vya kazi hivi karibuni na bado hawajalipwa posho zao za uhamisho.

Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ni kati ya Halmashauri hapa nchini zilizofanikiwa kutekeleza kwa wakati maelekezo ya Serikali ya kuwapandisha na kuwabadilishia vyeo watumishi wote waliostahili kwa mwaka 2021.



*Mtumishi wa TSC Wilaya ya Shinyanga, Elimeli Kabuga (kulia) akipokea cheti cha pongezi kwa kufanikisha zoezi la upandishaji na ubadilishaji vyeo watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.*

# TSC MISUNGWI YAKOSA USINGIZI, UDANGANYIFU WA MITIHANI



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (kulia) akiwa kwenye kikao na Watumishi wa TSC Wilaya ya Misungwi wakati wa ziara yake iliyofanyika katikati ya mwezi Oktoba 2021. Upande kushoto ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Misungwi, Manyanza Mageme.*

**Na Mwandishi wetu.**

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza, Manyanza Mageme ameeleza kuwa pamoja na walimu wa Wilaya hiyo kuendelea kuimarika katika nidhamu, makosa ya udanganyifu wa mitihani bado yanaendelea kushamiri.

Mageme ametoa kauli hiyo hivi karibuni wakati Jarida la Sauti ya TSC lilipomtembelea ofini kwa kwake kwa lengo la kujua maendeleo ya ofisi hiyo katika usimamizi wa ajira, maadili na maendeleo ya walimu ndani ya wilaya hiyo.

Mageme alisema kuwa kwa sasa suala la walimu kujiingiza katika udanganyifu wa mitihani linawanyima usingizi kwani licha ya kutoa elimu kuhusu maadili ya kazi ya ualimu bado ofisi yake ina mashauri mengi ya walimu wanaotuhumiwa kwa makosa hayo tofauti na miaka ya nyumba ambapo mashauri mengi yalihusu utoro.

"Ukiangalia mwaka jana na mwaka huu mashauri yanayohusu udanganyifu wa mitihani yamekuwa mengi tofauti na miaka ya nyuma. Kwa mwaka jana (2020/2021) tulikuwa na mashauri sita ya udanganyifu wa mitihani, mwaka huu (2021/2022) ambao hatujafika hata nusu yake tayari tuna mashauri sita



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Misungwi, Manyanza Mageme akiwa ofisini kwakwe.*

# TSC MISUNGWI YAKOSA USINGIZI, UDANGANYIFU WA MITIHANI

ya udanganyifu wa mitihani. Jambo hili linatuumiza kwani tunafanya jtihada kubwa katika kuwaelimisha walimu lakini bado vitendo hivi vinaendelea kutokea", alisema Mageme.

Kutokana na changamoto hiyo, Kaimu Katibu Msaidizi huyo alieleza kuwa ofisi yake imefanya ufuatiliaji ili kubaini kinachosababisha walimu kujiingiza katika makosa hayo licha ya kujua kuwa kufanya hivyo ni kosa la nidhamu na nikosa la jinai linaloweza kusababisha kupoteza ajira na kufungwa jela.

Alifafanua kuwa walibaini sabau kubwa ya kufanyika kwa makosa hayo kufanyika kuwa ni uutaratibu uliopo wa kuwatambua na kuwapongeza walimu hususan wakuu wa shule wanaofaulisha vizuri huku wale wasiofaulisha kujikuta katika hatari ya kuvuliwa madaraka ya




*Baadhi ya Watumishi wa TSC Misungwi wakiwa kwenye kikao na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani).*

ukuu wa shule.

"Ukiangalia utaratibu unaotumika sasa ni kuwa mkuu wa shule anayefaulisha wanafunzi vizuri anapewa maotisha lakini yule ambaye shule yake haikufaulisha yuko hatarini kuvuliwa madaraka. Sasa unakuta ikifikia kipindi cha mitihani wakuu wa shule wanatumia kila mbinu kuhakikisha wanafunzi wanafaulu ili aendelee kulinda nafasi yake" alisema Mageme.

Hivyo, anashauri kuwa ni vyema ukaandaliwa utaratibu ambao hautawachochea walimu kujiingiza katika vitendo vya udanganyifu wa mitihani kutokana na hofu ya kuondolewa kwenye nyadhifa zao.

Kuhusu hali ya kinidhamu kwa ujumla katika Wilaya hiyo, Mageme alilieleza Jarida hili kuwa mashauri yamepungua ikilinganishwa na miaka ya nyuma kitu kinachoashiria kuwa walimu wamepata elimu ya kutosha kuhusu taratibu mbalimbali za utumishi wao.

Elieleza kuwa ofisi yake imekuwa ikishirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmasahauri ya Wilaya ya Misungwi katika kufanya ziara shuleni na



*Baadhi ya Watumishi wa TSC Misungwi wakiwa kwenye kikao na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani).*

# TSC MISUNGWI YAKOSA USINGIZI, UDANGANYIFU WA MITIHANI

kukutana na walimu kwa lengo la kuwaelimisha juu ya Sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za utumishi wa Umma.

"Tunafanya kazi vizuri na Maafisa Elimu katika Halmashauri hii, pale wanapokuwa na ziara shuleni tunakwenda pamoja na wakati mwingine kunapokuwa na changamoto za kinidhamu kwa walimu wanaofundisha kwenye shule binafsi wanatuita kwa ajili ya kuwasaidia ushauri," alisema.

Akizungumzia masuala ya ajira na maendeleo ya walimu, Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema kuwa Wilaya hiyo ina jumla ya walimu 2,160 ambapo katika idadi hiyo walimu 1,564 ni wa shule za msingi na 596 ni wa shule za sekondari.

Aliendelea kueleza kuwa katika ajira mpya zilizotoka mwezi Desemba 2020 na Julai 2021 Wilaya hiyo ilipatiwa walimu 91 ambapo katika idadi hiyo walimu 88 walisajiliwa, walimu wawili hawakuripoti katika vituo vya kazi walivyopangiwa na mwalimu mmoja hakusajiliwa kutokana kuwepo kwa mkanganyiko wa majina katika vyeti vyake.

Kwa upande wa upandishaji madaraja, Magene alieleza kuwa ofisi yake ilipandisha jumla ya walimu 773 ambapo walimu 479 ni wa shule za msingi na walimu 294 ni wa shule za sekondari na hadi kufikia mwezi Septemba 2021 walimu wawili tu ndio walikuwa hawajabadilishiwa mishahara yao kutokana na sababu mbalimbali.

Hata hivyo, Mageme alilieleza kuwa jitihada mbalimbali zimeendelea kufanyika kati ya Ofisi yake, Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya pamoja na Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili watumishi hao waweze kubadilishiwa mishahara yao.

Pamoja na idadi hiyo ya waliopandishwa madaraja, walimu watatu hawakupandishwa kwa kuwa walikuwa na mashauri ya nidhamu hiyo walikosa sifa kutokana na mwongozo uliotolewa na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika zoezi hilo.



*Picha ya pamoja kati ya watumishi wa TSC Misungwi na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (wa tatu kutoka kulia).*

# PROF. KOMBA AWATAKA KAIMU KATIBU WASAIDIZI WA TUME NCHINI KUFIKIA MATARAJIO YA OFISI YA RAIS – IKULU KATIKA RUFAA ZA UAMUZI WA MASHAURI YA WALIMU

**Na Mwandishi Wetu**

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Prof. Willy Komba, amewataka Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka wilaya 139 nchini kuzingatia na kuyafikia matarajio ya Ofisi ya Rais – Ikulu katika kufanyia kazi rufaa zinazokatwa dhidi ya uamuzi wa Tume kwa kuzingatia yote yaliyoelekezwa katika kushughulikia mashauri ya nidhamu katika ngazi za wilaya ili kupunguza rufaa hizo zinazokatwa katika ngazi ya Tume Makao Makuu na Ofisi ya Rais – Ikulu.

"Pamoja na hilo nawakumbusha na kuwasisistiza kuendelea kuunga mkono na kutekeleza maagizo ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuchukua tahadhari na kuwakumbusha walimu na wanafunzi katika maeneo yao kuchukua tahadhari dhidi ya UVIKO-19 ikiwa ni pamoja na kuhamasishana kupata chanjo kwa ajili ya kulinda afya zetu na jamii zetu kwa ujumla." Alisema Prof. Komba

Prof. Komba aliyasema hayo hivi karibuni akifunga Kikao Kazi cha Katibu wa Tume, Mwalimu Paulina Nkwama, ndc na Kaimu Katibu Wasaidizi hao kilichofanyika kwa siku mbili Mkoani Dodoma ili kupeana taarifa mbalimbali za utekelezaji, kukumbushana baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba akitoa neno la kumkaribisha Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde ili afungue Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka wilaya 139 za Tanzania Bara kilichafanyika Oktoba 21-22, 2021 jijini Dodoma.*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde (kushoto), Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (katikati) na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kushoto) wakitoka kwenye ukumbi wa Chuo cha Mipango, Dodoma.*

# PROF. KOMBA AWATAKA KAIMU KATIBU WASAIDIZI WA TUME NCHINI KUFIKIA MATARAJIO YA OFISI YA RAIS – IKULU KATIKA RUFAA ZA UAMUZI WA MASHAURI YA WALIMU





*Badhi ya Washiriki wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka wilaya 139 za Tanzania Bara wakichangia mada wakati wa mkuano huo.*

Tume, na kujengeana uwezo katika maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu wa weledi kiutendaji wa majukumu ya siku kwa siku.

Mwenyekiti Prof. Komba aliwakumbusha kuzingatia ushughulikiaji wa masuala ya nidhamu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, na Taratibu kwani Katibu Msaidizi Wilayani ndiye msimamizi wa haki za walimu anaowahudumia hivyo ni vema kuzingatia Sheria na kutoa haki kwa uadilifu wakati wa kutoa maamuzi ya mashauria ya nidhamu na maadili kazini.

Aidha alisema pamoja na kupewa ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu walimu, ni wazi hiyo itasaidia wao kujipanga vyema katika kutekeleza majukumu kwa ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati ya namna ya kuwakumbusha walimu kuhusu maadili na miiko ya kazi yao na hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa idadi ya walimu wanaoadhibiwa kwa kukiuka maadili ya kazi ya ualimu.

Akizungumzia enao la Utawala Bora Prof. Komba alisema ni jukumu la wajumbe wote wa kikao hicho kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa kuzingatia misingi ya utawala bora ikiwa ni pamoja na kuepuka kutengeneza mazingira rushwa au vitendo vya kupokea rushwa ambavyo vinadidimiza haki za watumishi wanaowahudumia.

Vilevile, kwa niaba ya Tume na Uongozi wake aliahidi kuzifuatilia na kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoikabili Tume Makao Makuu na Wilayani kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wadau wengine wa Elimu nchini.

Hali kadhalika Mwenyekiti huyo wa Tume alizitaja ndoto nne za Tume kuwa ni pamoja na; kuwajengea uwezo Kaimu Katibu Wasaidizi wote katika kutekeleza majukumu yao hii ikiwa ni pamoja na wajumbe wa kamati za Tume, fursa za mafunzo endelevu kuratibiwa vizuri kitaifa, Tume kujengewa uwezo wa kufanya utafiti ili kutoa ushauri wenye mashiko kwa Sekta na Taifa, pamoja na kuboresha miundombinu ya TEHAMA ikiwa ni moja ya majibu kwa tabia mbaya ya kutoa huduma kwa upendeleo na rushwa.

Kabla ya kufunga kikao kazi hicho aliwakumbusha na kuwasisitiza wajumbe wote kutoa ushirikiano kwa wataalamu watakaofika kwenye maeneo yao kwa ajili ya zoezi la Sensa ili kutimiza adhma ya Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo hii ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Mhe. Rais baada ya hivi karibuni kuzindua Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa ya Makazi na Watu yam waka 2022.

# USHIRIKIANO WA KARIBU WA TSC NA WAKURUGENZI WA MAJIJI, MANISPAA, HALMASHAURI ZA WILAYA NA MIJI WALETA HUDUMA BORA NA KUPUNGUZA MALALAMIKO YA WALIMU NCHINI



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde akitoa hotuba ya ufunguzi wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutoka wilaya 139 za Tanzania Bara. Kikao hicho kilifanyika Oktoba 21-22, 2021 jijini Dodoma.*

**Na Mwandishi Wetu**

Ushirikiano wa karibu uliopo kati ya Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Walimu (PO-TSC) na Ofisi za Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa, Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Miji kupitia Idara za Elimu Msingi na Sekondari umesaidia sana walimu kupata huduma zinazostahili kwa wakati na hivyo kupunguza malalamiko miongoni mwao.

Hilo limesemwa hivi karibuni na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, wakati alipokua akifungua Kikao Kazi cha Tume na Kaimu Katibu Wasaidizi kilichofanyika kwa siku mbili Mkoani Dodoma ili kupeana taarifa mbalimbali za utekelezaji, kukumbushana baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Tume, na kujengeana uwezo katika maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu wa weledi kiutendaji wa majukumu ya siku kwa siku.

Pamoja na hilo Naibu Waziri Silinde ameipongeza Tume Makao Makuu na Wilayani kwa kazi nzuri iliyotekelezwa ya kuwapandisha madaraja walimu katika zoezi lililofanyika mwezi Mei na Juni, 2021 kwani hiyo imetokana na uelewa wa masuala ya kiutumishi yanayoleta mabadiliko chanya katika kuwahudumia walimu katika ngazi zote makao makuu na wilayani.

"Ni matumaini yangu kuwa, kikao kazi hiki kitakua na mchango mzuri wa mawazo ili kutoa mikakati mizuri ambayo tutaweza



*Badhi ya washiriki wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka wilaya 139 za Tanzania Bara kilichafanyika wakiwa katika hali ya utulivu wakati kikao hicho kinaendelea.*



*Badhi ya washiriki wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka wilaya 139 za Tanzania Bara kilichafanyika wakiwa katika hali ya utulivu wakati kikao hicho kinaendelea.*

# USHIRIKIANO WA KARIBU WA TSC NA WAKURUGENZI WA MAJIJI, MANISPAA, HALMASHAURI ZA WILAYA NA MIJI WALETA HUDUMA BORA NA KUPUNGUZA MALALAMIKO YA WALIMU NCHINI



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kulia), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) pamoja na Wajumbe wa Menejimenti ya TSC wakati wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka wilaya 139 za Tanzania Bara kilichafanyika Oktoba 21-22, 2021 jijini Dodoma.*

kuitumia katika utekelezaji wa kila siku wa majukumu yetu na kuisaidia Tume kusimamia vyema maadili ya Walimu na kuchukua hatua stahiki kwa walimu watakaobainika kukiuka maadili ya kazi yao." Alisema Mhe.Silinde

Alisema Katibu Wasaidizi kwa mujibu wa majukumu yao wanatakiwa kutenda haki na hivyo Serikali haitarajii kuona au kusikia wanajiingiza katika vitendo vinavyoashiria ubadhirifu, udhalilishaji, rushwa, uvunjaji wa Sheria, Taratibu na Kanuni kwa kuacha vitendo vya uonevu hasa wakati wa upandishaji madaraja, mashauri ya nidhamu na kubambikiza makosa walimu.

Aidha Mhe. Silinde alisema changamoto ya uteuzi wa Katibu Wasaidizi wa Wilaya inafanyiwa kazi tangu lilipowasilishwa na kuchukuliwa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ummy Mwalimu, wakati akifungua Kikao cha Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume na aliahidi majibu ya changamoto hiyo kupatikana kwa wakati.

Vilevile alisema Serikali imepokea changamoto zote za Tume na aliahidi kuzingatiwa na kupatiwa ufumbuzi katika mipango ya bajeti ya wizara yam waka unaofuata 2021/2022 huku akiwataka Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa, Halmashauri za Wilaya na Miji kutenga ofisi zenye hadhi kwa Tume ya Utumishi wa Walimu na kutumia magari ya Idara ya Elimu kwa maafisa wa Tume kila itakapoonekana inafaa.

Hali kadhalika Mhe. Silinde kupitia Kikao Kazi hicho aliwasisitiza wajumbe wote kutoa ushirikiano kwa wataalamu watakaofika kwenye maeneo yao kwa ajili ya zoezi la Sensa ili kutimiza adhma ya Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo hii ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Mhe. Rais baada ya hivi karibuni kuzindua Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa ya Makazi na Watu yam waka 2022.

Kikao kazi hicho kilihudhuriwa na Kaimu Katibu Wasaidizi kutoka Wilaya 139 Tanzania Bara, Safu ya Uongozi na baadhi ya Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu.



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kulia), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) baadhi ya Kaimu Katibu Wasaidizi walioshiriki Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka wilaya 139 za Tanzania Bara kilichafanyika Oktoba 21-22, 2021 jijini Dodoma.*

# TSC YAPATA MEDALI SHIMIWI, RIADHA WAZEE




*Mchezaji wa riadha, Bitwalihati Magota akivalishwa medali baada ya kushika nafasi ya tatu kwenye mbio za mita mia moja zilizohusisha watumishi wa umma wenye umari wa kuanzia miaka 55.*




*Mchezaji wa riadha, Bitwalihati Magota akipongezwa baada ya kupata medali kwa kushika nafasi ya tatu kwenye mbio za mita mia moja zilizohusisha watumishi wa umma wenye umari wa kuanzia miaka 55.*



*Wachezaji walioshika nafasi ya kwanza hadi ya tatu (waliosimama nyuma) wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa SHIMIWI waliowavalisha medali baada ya kuibuka washindi kwenye mbio za mita mia moja upande wa wazee.*



*Mchezaji wa riadha, Bitwalihati Magota kutoka TSC akionesha medali yake aliyoipata baada ya kushika nafasi ya tatu kwenye mbio za mita mia moja zilizohusisha watumishi wa umma wenye umari wa kuanzia miaka 55.*

**Na. Mwandishi Wetu**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imepata medali kwenye mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) inayofanyika mkoani Morogoro baada ya kushika nafasi ya tatu kwenye mchezo wa riadha unaohusisha watumishi wenye umri wa kuanzia miaka 55.

TSC iliwakilishwa na mchezaji wake, Bitwalihati Magota ambaye ndiye amekuwa mchezaji wa kwanza kutwaa medali kwa upande wa wachezaji wa TSC kwenye mashindano hayo ambayo yanatarajiwa kumalizika Novemba 2, 2021 baada ya kufanyika kwa muda wa wiki mbili.




*Picha inayowaonesha wachezaji wa riadha kwa mbio za mita mia moja upande wa wazee wakiwa tayari kuanza mchezo huo.*

# TSC IWEZESHWE KUTEKELEZA MAJUKUMU YAKE: MKURUGENZI JIJI MWANZA

**Na. Mwandishi Wetu**

Mkurugenzi wa jiji la Mwanza, Sekiete Yahaya ameeleza kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ni chombo muhimu ambacho kinapaswa kufanya kazi zake kwa uhuru bila kuingiliwa na mamlaka zingine ili kutenda haki hususan pale inaposhughulikia masuala ya nidhamu ya walimu.

Mkurugenzi huyo ameyasema hayo hivi karibuni wakati Jarida la Sauti ya TSC lilipofika ofisini kwake na kufanyanya mahojioano juu ya masuala mbalimbali yanayohusu walimu katika Jiji hilo lenye utajiri wa Samaki kutoka Ziwa Viktoria.

Alieleza kuwa Ofisi za TSC ngazi ya Wilaya zinapaswa kuendelea kuwezeshwa ili ziweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo ikiwa ni pamoja na kupatiwa fedha kwa ajili ya kuendeshesha vikao vya kamati ambavyo ndivyo vinavyotoa uamuzi wa masuala mbalimbali ya walimu.

"Sisi waajiri tunapomripoti mwalimu TSC kwasabau ya kukiuka maadili ya kazi yake, tunatarajia kuwa mwalimu yule ataadhibiwa. Lakini tunajua kuwa TSC nao kwa mamlaka waliyopewa wanaendesha shauri na hatimaye wanatoa uamuzi. Sasa unaweza ukaona kama TSC itakuwa haina uwezo kifedha na ikawa inamtegemea Mkurugenzi aiwezeshe kutekeleza majukumu yake, kuna uwezekano mkubwa ikawa inatoa uamuzi unaoegemea upande mmoja na kukiuka haki ya upande mwingine," alisema Yahaya.

Mkurugenzi huyo alieleza kuwa kwa upande wa ofisi yake, inaitambua TSC na kumekuwa na ushirikiano wa ukaribu baina ya ofisi hizo katika kutekeleza majukumu mbalimbali yanayohusu walimu na ameahidi kuendela kutoa ushirikiano ili kutatua changamoto za walimu kwa wakati ili nao waweze kufundisha wanafunzi kwa ufanisi.

"Mimi naifahamu vizuri sana TSC, kabla ya kuwa mkurugenzi nilikuwa Afisa Utumishi na nilikuwa nafanya kazi kwa karibu na TSC, hivyo hata sasa bado ninatoa ushirikiano sana kwa Tume. Wakati wowote wanapokuja kwangu wakiwa na mambo yao tunakaa tunajadili na tunapata ufumbuzi. Lengo hapa ni kuhakikisha tunaondoa kero na malalamiko ya walimu kwa kadri inavyowezekana," alisema.

Wilaya ya Nyamagana ina jumla ya shule za Serikali 110 ambapo shule 80 ni za msingi na 30 ni za sekondari huku idadi ya walimu wanaofundisha shule hizo ni 3643, katika idadi hiyo walimu 2387 ni wa shule za msingi na walimu 1286 ni wa shule za



*Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Sekiete Yahaya akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mwasiliano ya Serikali kutoka TSC, Gerard Chami (kulia) pamoja na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Nyamgana, Peninah Byangwan (kushoto) ofisini kwake jijini Mwanza hivi karibuni.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Nyamgana, Peninah Byangwan akiwa ofisini kwake.*

# TSC IWEZESHWE KUTEKELEZA MAJUKUMU YAKE: MKURUGENZI JIJI MWANZA

sekondari.

Kwa mujibu wa Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC katika Wilaya hiyo, Peninah Byangwan zoezi la upandishaji madaraja na kuwabadilishia vyeo walimu waliojiendeleza kielimu lilikwenda vizuri ambapo jumla ya walimu 1150 walipandishwa madaraja na kubadilishiwa mishahara yao na huku walimu 58 wakibadilishiwa vyeo.

Kwa upande wa nidhamu, katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2021 jumla ya mashauri 9 ya nidhamu yalifunguliwa ambapo mashauri 4 ni ya walimu wa shule za msingi na 5 ni ya walimu wa sekondari.

"kwa ujumla hali ya nidhamu kwa walimu wa Wilaya ya Nyamagana ni nzuri, hata ukiangalia mashauri ya nidhamu yanaendelelea kupungua ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Hii ni kwasababu tumefanya ziara za mara kwa mara shuleni, tumekutana na walimu na kuwakumbusha masuala ya msingi ya utumishi wao", alisema Peninah.

Pamoja na hali ya nidhamu kuwa nzuri, Kaimu Katibu Msaidizi huyo anabainisha kuwa kumekuwa na changamoto ya walimu kutaka mafanikio makubwa kwa haraka na kujikuta wakirubuniwa na kutapeliwa kwa kushawishiwa watoe fedha huku wakiaminishwa kuwa watapata faida kubwa.

"Kuna mwalimu mmoja alikuwa haendi kwenye kituo chake cha kazi kufundisha, badala yake anapita kwenye shule mbalimbali kuhamasisha walimu watoe fedha kujiunga na hizo biashara za upatu. Kwa hapa bado tunakazi ya ziada katika kuwaelimisha walimu kwa kuwa pamoja na kuwaeleza sana, kila kukicha unasikia wametapeliwa," alisisitiza.

Changamoto nyingine inayowakabili walimu katika wilaya hiyo ni kukopa kupita kiasi. Peninah anaeleza kwamba walimu wanakopa kwenye mabenki na taasisi nyingine za kifedha hadi wanafikia ukomo wa kukopa kwa mujibu wa sheria, wakishaona kwenye mikopo rasmi hakopesheki wanakwenda mitaani kwa watu binafsi kukopa tena.

"Utakuta mwalimu akipokea mshahara wote unaishia kwenye kulipa madeni, anashindwa kuja shuleni maana hata nauli hana wala hela ya kula mchana hana. Kinachotokea unakuta mwalimu anaanza kuwa mtoro na hatimaye anakuja kufukuzwa kazi," alieleza Peninah.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo anahitimisha kwa kueleza kuwa ofisi yake inaendelea kufanya vikao mbalimbali na walimu, chama cha walimu, pamoja na wadu wengine ili kuongeza msisitizo wa kuwakubusha walimu umuhimu wa kulinda ajira zao kwa kuzingatia taratibu za kiutumishi.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Nyamgana, Peninah Byangwan (kushoto) akielezea maendeleo ya ofisi yake katika kuwahudumia walimu. Pembeni yake ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gererd Chami.*




*Watumishi wa TSC Wilaya ya Nyamagana wakiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gererd Chami (watatu kutoka kushoto) wakati Chami alipotembelea ofisi za TSC Nyamagana hivi karibuni.*

# KAMATI ZA UJENZI CHAMWINO ZATAKIWA KUSIMAMIA MIRADI KWA UADILIFU



*Kikao kilichowakutanisha Wajumbe wa Kamati za Ujenzi za Shule kikiwa kinaendelea.*

**Na Mwandishi Wetu**

Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya, amekutana na Kamati za Ujenzi za Kata 28 za Wilaya hiyo kwa ajili ya kuweka mikakati ya kuweza kukamilisha miradi ya elimu kwa wakati ambapo Wilaya ya Chamwino imepatiwa jumla ya Tsh. 2,920,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Madarasa 82 ya Sekondari na Shule shikizi 64.

Katika kiako hicho, Msuya alizitaka kamati hizo kufanya kazi kwa uadilifu na kuhakikisha kuwa ifikapo tarehe 15.12.2021 miradi yote iwe imekamilika huku akitaka kamati hizo kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa ubora unaotakiwa kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.

Aliongeza kuwa kila kamati ihakikishe inafanya kazi kwa ushirikiano huku kila mmoja akitimiza wajibu wake na kueleza kuwa hatavumilia uzembe wa aina yoyote katika matumizi ya fedha na usimamizi wa miradi hiyo.

Wakati huo huo, Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Chamwino, Paulina Kanumba amewataka walimu wanaohusika na usimamizi wa miradi hiyo kuhakikisha wanazingatia miiko na maadili ya kazi ya ualimu ili kujiepusha na vitendo vya ukiukaji wa maadili vitakavyosababisha wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Paulina aliwasisitiza wajumbe hao kuwa pale wanapoķutana na changamoto wakati wa utekelezaji wa miradi, watoe taarifa kwa viongozi ili ufumbuzi wa haraka upatikane badala ya kufanya kitu wasichokuwa na ukahika nacho na baadaye kujikuta wameingia kwenye matatizo.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Chamwino, Paulina Kanumba akiongea na wajumbe wa Kamati za Ujenzi kuhusu kuzingatia Miiko na Maadili ya Kazi ya ualimu katika Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi ya shule.*



*Baadhi ya wajumbe waliohudhuria kikao cha Kamati za Ujenzi za Shule katika Wilaya ya Chamwino kilichofanyika hivi karibuni wilayani hapo wakiwa wanaendelea kufuatilia kilichokuwa kinaendelea wakati wa kikao hicho.*

# Wakuu wa Shule hawatekelezi Wajibu wao ipasavyo: Fundikira

**Na Mwandishi Wetu.**

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ilemela, James Fundikira amesema wakuu wa shule wilayani hapo bado hawajatekeleza majukumu yao kama mamlaka ya kwanza ya nidhamu kwa walimu kitu ambacho kinasababisha kutochukuliwa hatua za udhibiti nidhamu ya walimu kwa wakati.

Fundikira ameyasema hayo hivi karibuni wakati Jarida hili lilipofika ofisini kwakwe kwa lengo la kutaka kujua maendeleo ya Ofisi ya ofisi hiyo katika kuwahudumia walimu kwenye masuala ya Ajira, Maadili na maendeleo katika utumishi wa walimu.

Fundikira alianza kwa kueleza kuwa wilaya hiyo ina jumla ya walimu 2510 wanaoufundisha shule za msingi na sekondari za serikali, katika idadi hiyo walimu 1474 ni wa shule za msingi na 1036 ni wa shule za sekondari huku idadi ya shule za msingi ikiwa ni 76 na sekondari 28.

Aliendelea kueleza kuwa ili kupunguza mashauri ya nidhamu kwa walimu ni lazima wakuu wa shule wanafanye kazi ya kusimamia walimu kikamilifu na pale inapotokea mwalimu anaanza kwenda kinyume na maadili ya kazi aweze kurekebishwa mapema badaya ya kukaa na kusubiri kosa liwe kubwa ili mkuu wa shule aliripoti kwa mwajiri.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ilemela, Fundikira James (kushoto) akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami wakati Mkuu huyo wa Kitengo alipotembelea ofisi za TSC Ilemela hivi karibuni.*



*Watumishi wa TSC Ilemela wakiwa katika kikao na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami katika ofisi za TSC Ilemela.*

"Kama tunavyojua, kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2025 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2016 wakuu wa shule ndiyo mamlaka ya kwanza ya nidhamu kwa walimu, hivyo wanapaswa kuwasaidia walimu kwa kuwaelimisha juu ya miiko na maadili ya kazi hiyo," alisema Fundikira.

Aliendelea kusema, "wakuu wa shule hawachukui hatua pale walimu wanapokwenda kinyume na baadili, badala yake tunaletewa kesi ambazo ukiangalia zilipaswa zishughulikiwe na kumalizwa kwenye ngazi ya shule. Hapa kwetu bado tuna kazi ya kufanya katika kuwasaidia wakuu wa shule watekeleze majukumu yao ya mamlaka ya nidhamu kama inavyotakiwa."

Alifafanua sababu zinazosababisha wakuu kutochukua hatua za nidhamu kuwa ni kuogopa kuchukiwa na walimu, wakati mwingine wakuu wa shule wakiwa wakali walimu wanalalamika kwa afisa

# Wakuu wa Shule hawatekelezi Wajibu wao ipasavyo: Fundikira



*Watumishi wa TSC Ilemela wakiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (wa pili kutoka kulia) wakati Chami alipofanya ziara katika ofisi hiyo hivi karibuni.*




*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ilemela, Fundikira James akiwa katika sehemu maalum iliyotengwa kwa ajili ya TSC kuegesha vyombo vyake vya usafiri.*

elimu kuwa mkuu wa shule anawanyanyasa.

"Tulichogundua ni kwamba hawa wakuu wa shule wanaogopa kuchukiwa na walimu, kwa hiyo mwalimu akifanya kosa anamuacha tu akiona amezidi anatoa taarifa kwa afisa elimu ili sisi tumchukulie hatua lakini yeye hataki kuchukua hatua. Wakati mwingine mkuu wa shule akiwa ni mkali katika kusimamia nidhamu, walimu wanaona kuwa anawanyanyasa na wanapeleka malalamiko kwa afisa elimu ambaye anaweza akaamua kumvua madaraka mkuu wa shule," alieleza.

Fundikira aliendelea kueleza kuwa pamoja na kuwa nidhamu ya walimu wilayani hapo ni nzuri, bado kuna changamoto ya utoro ambao kwa kiasi kikubwa unasababishwa na baadhi ya walimu hasa vijana kujishughulisha na kazi nyingine za maendeleo wakati wa masaa ya kazi.

"Unajua hapa mjini kuna shughuli nyingi za kufanya za kujiletea maendeleo. Sasa unakuta mwalimu anaanzisha biashara yake na akiona inakwenda vizuri, haendi tena shuleni kufundisha. Tumekaa na walimu mara nyingi na tumewaeleza kuwa kufanya biashara ni jambo jema lakini lazima tuzifanye nje ya muda wa kazi," alisema.

Alihitimisha kwa kusema kuwa ofisi yake inaendelea kufanya jitihada mbalimbali za kukutana na walimu, kuzungumza nao na kuwapa ushauri wa namna ya kufanya shughuli zao za maendeleo bila kuathiri taratibu za utumishi wao ili wasijikute wanaingia kwenye matatizo ya kinidhamu.



*Wachezaji wa mpira wa pete kutoka TSC (wenye soksi za rangi ya njano na kijani) wakiwa uwanjani kwenye mashindano ya Shimiwi.*



*Wachezaji wa mpira wa pete kutoka TSC (wenye soksi za rangi ya njano na kijani) wakiwa uwanjani kwenye mashindano ya Shimiwi.*



*Wachezaji wa kuvuta kamba kwa upande wa wanawake wakiwa kwenye mchezo huo wakati wa mashindano ya SHIMIWI mkoani Morogoro.*



*Wachezaji wa mchezo wa kuvuta kamba kutoka TSC kwa upande wa wanaume wakivuta kamba wakati wa mashindano ya SHIMIWI mkoani Morogoro.*



*Mchezaji wa TSC, Flora Chanda (aliyesuka) akicheza karata katika mashindano ya SHIMIWI mkoani Morogoro.*



*Mchezaji wa TSC, Silver Igogo (wa kwanza upande wa kulia) akicheza karata katika mashindano ya SHIMIWI mkoani Morogoro.*



*Wachezaji wa kuvuta kamba upande wa wanaume kutoka TSC wakishangilia ushindi baada ya kufanikiwa kuivuta timu ya Wizara ya Ulinzi katika mashindano ya SHIMIWI mkoani Morogoro.*

# WALIMU 927 KATI YA 935 WAPANDISHWA VYEO NA ASILIMIA 85 YA MASHAURI YA NIDHAMU YALIHITIMISHWA WILAYANI NZEGA 2020/2021

**Na Mwandishi Wetu.**

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilayani Nzega Ndg. Leonard Japhet, amesema katika kipindi cha mwaka 2020/2021 jumla ya walimu 927 walipandishwa cheo kati ya 935 waliostahili; ikiwa ni walimu 673 wa Shule za Msingi na 254 wa Shule za Sekondari ambapo matazamio katika kipindi cha mwaka 2021/2022 ni kupandisha cheo walimu wengine 509 wa Shule za Msingi na Sekondari wilayani humo.

Alisema jumla ya walimu nane kati ya walimu 935 waliostahili kupandishwa cheo hawakupandishwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo; kuwa na mashauri ya kinidhamu na maadili yanayoendelea na wengine kuwemo katika kipindi cha kutumikia adhabu zao za kinidhamu na maadili.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi huyo alipokua akifanya mahojiano na Maafisa wa Mawasiliano ya Serikali na Habari kutoka Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Walimu (PO-TSC) Makao Makuu waliokua katika ziara ya kikazi kutembelea ofisi za TSC katika Wilaya za Nzega, Shinyanga, Misungwi, Nyamagana, na Ilemela kupata habari za utekelezaji wa majukumu ya Tume wilayani.

"Pamoja na walimu hao 927 kati ya 935 waliopandishwa cheo, katika mwaka wa fedha 2020/ 2021 na 2021/ 2022 jumla ya mashauri ya nidhamu 20 yalipokelewa na mashauri 17 kati ya hayo yalihitimishwa kwa wahusika kupewa onyo,



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali TSC, Gerard Chami (kushoto) akiongea na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Nzega, Leonard Japhet juu ya masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu katika wilaya hiyo.*



*Mtumishi wa TSC Nzega, Andrew Mabala akiwa anaendelea kutekeleza majukumu yake ya kila siku ofisini kwake.*



*Mtumishi wa TSC Nzega, Alice Nshunju akiwa anaendelea kutekeleza majukumu yake ya kila siku ofisini kwake.*



*Mtumishi wa TSC Nzega, Florah Paschal akiwa anaendelea kutekeleza majukumu yake ya kila siku ofisini kwake.*



*Mtumishi wa TSC Nzega, Catherine Shija akiwa ofisni kwake.*

# WALIMU 927 KATI YA 935 WAPANDISHWA VYEO NA ASILIMIA 85 YA MASHAURI YA NIDHAMU YALIHITIMISHWA WILAYANI NZEGA 2020/2021



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Nzega wakiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali TSC, Gerard Chami wakati Mkuu huyo wa Kitengo alipotembelea ofisi ya TSC Nzega hivi karibuni.*

kushushwa cheo, kufukuzwa kazi, na wengine kubainika kutokua na hatia hivyo kurejeshwa kazini." Alisema Japhet

Aidha, Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema sehemu ya mashauri ya kinidhamu yalikuwa ya makosa ya utoro na ulevi ambayo kwa sehemu kubwa yanawahusisha walimu vijana ambao wengi wao wanakua na matarajio makubwa tofauti na hali halisi na hivyo kuiomba Serikali kurejesha Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ambayo yanaweza kusaidia vijana kupunguza au kuondokwa kabisa na matarajio hayo mara wanapoajiriwa.

Katika kuhakikisha nidhamu na maadili ya kazi ya ualimu yanaimarika wilayani Nzega alisema ofisi yake imezipatia shule zote wilayani hapo vitabu vya maadili ya kazi ya ualimu kwa ajili ya rejea na kujenga uelewa zaidi kwa walimu wawapo katika utekelezaji wa majukumu yao shuleni na maeneo mengine ya jamii wanazoishi na kuchangamana nazo.

Vilevile Kaimu Katibu Msaidizi Japhet alisema jumla ya walimu 91 wa Shule za Msingi na Sekondari walioajiriwa katika kipindi cha mwaka 2020/ 2021 wanatarajiwa kuthibitishwa kazini siku za karibuni baada ya kukidhi kiwango tarajiwa cha utoaji huduma ikiwa ni pamoja na jumla ya walimu 28 kubadilishwa cheo kati ya 42 walioomba huku waliosalia wakisubiri mapitio ya muundo hasa eneo la ngazi za mshahara ili nao wabadilishwe.

Akirejea mgawanyo wa walimu wilayani humo Kaimu Katibu Msaidizi Japhet alisema wilaya ina jumla ya walimu 2,589 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ina jumla ya walimu 1997 (Shule za Msingi 1,547 na Sekondari 450) huku Halmashauri ya Mji wa Nzega ikiwa na jumla ya walimu 592 (Shule za Msingi 444 na Sekondari 148).

Wilaya ya Nzega kwa ujumla wake ina shule 222 ambapo Shule za Msingi ni 180 na Sekondari 42 huku Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ikiwa na jumla ya Shule 180 (Shule 149 za Msingi na 31 za Sekondari) na Halmashauri ya Mji wa Nzega ikiwa na jumla Shule 42 (Shule 31 za Msingi na 11 za Sekondari).



# TSC YAFANYA MAPITIO YA MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akifungua kikao cha kufanya mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa TSC kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma. Pembeni yake ni Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa TSC, Moses Chitama.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiongoza kikao cha kufanya mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa TSC kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*



*Baadhi ya washiriki wa kikao cha kufanya mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa TSC wakiwa kwenye kikao.*



*Baadhi ya washiriki wa kikao cha kufanya mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa TSC wakiwa kwenye kikao.*



*Baadhi ya washiriki wa kikao cha kufanya mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa TSC wakiwa kwenye kikao.*

# CWT, MANISPAA NA HALMASHAURI YA WILAYA SHINYANGA WATUNUKU HATI ZA PONGEZI KWA WATUMISHI WA OFISI YA TSC WILAYA KUFANIKISHA UPANDISHAJI VYEO WALIMU

**Na Mwandishi wetu.**

Chama cha Walimu pamoja na Halmashauri zote za Wilaya ya Shinyanga zimeipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wilayani hapo pongezi zilizoendana na kukabidhiwa kwa hati za pongezi kwa kushiriki na kufanikisha kwa kiwango cha juu upandishaji cheo kwa walimu wanaotumikia katika Manispaa ya Shinyanga na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Shinyanga Mwalimu Happiness Mlangi mbele ya Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi katika Manispaa ya Shinyanga Ndg. Getrude Gisema wakati wa mahojiano na Maafisa wa Mawasiliano ya Serikali na Habari kutoka Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Walimu (PO-TSC) Makao Makuu waliokua katika ziara ya kikazi kutembelea ofisi za TSC Wilaya za Nzega, Shinyanga, Misungwi, Nyamagana, na Ilemela ili kupata habari za utekelezaji wa majukumu ya Tume wilayani.

"Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 jumla ya walimu 1,090 kati ya walimu 2,576 wanaohudumu katika Manispaa ya Shinyanga (917) na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (1,659) walipandishwa cheo na kati ya waliopandishwa; 545 wanahudumu katika Manispaa ya Shinyanga na 545 wanahudumu katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ambao pia wote wameanza kupokea mishahara mipya baada ya kupandishwa vyeo walivyostahili." Alisema Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilayani Shinyanga Mwalimu Happiness Mlangi



*Afisa Utumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Getruda Gisema akitoa neno fupi wakati wa hafla ya kuipongeza timu ya watumishi waliofanikisha zoezi la kupandisha madaraja na kubadilisha vyeo watumishi wa Manispaa hiyo. Hafla hiyo imefanyika hivi karibuni katika Manispaa ya Shinyanga.*

Kaimu Katibu Msaidizi huyo amesema Idara ya Elimu katika Manispaa na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga zimekua zikiwashirikisha sana katika masuala mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu ya kisekta ikiwa ni pamoja na kutoa mada za kujengeana uwezo na kukumbushana mambo mbalimbali yanayohusu majukumu ya Kisheria ya TSC ambayo ni; Ajira, Nidhamu, na Maadili katika Utumishi wa Walimu nchini.

Aidha alisema katika kipindi cha mwezi mmoja wa Oktoba, 2021 mashauri ya nidhamu kwa walimu katika Manispaa na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga yamepungua kutoka wastani wa saba ya awali mpaka wastani wa upokeaji wa mashauri ya nidhamu chini ya matano ambao kwa mwezi tajwa wa Oktoba ni mashauri ya nidhamu matatu tu ndiyo yaliyopokelewa ikiwa mawili yanatokea Manispaa ya Shinyanga na moja kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ambapo yote yapo katika hatua ya uchunguzi yakihusishwa na utoro, kukiuka maadili, na kughushi vyeti.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Shinyanga inahudumia jumla ya shule za msingi na sekondari 234 ambapo Manispaa ya Shinyanga ina jumla ya shule 70 (48 Msingi, 18 Sekondari, na 4 Shikizi) huku Halmashauri ya Wilya ya Shinyanga ikiwa na jumla ya shule 164 (136 Msingi na 28 Sekondari).

# TSC Shinyanga, Ofisi inayohudumia Halmashauri Mbili

**Na Mwandishi Wetu.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Shinyanga ni moja ya ofisi zinazohudumia walimu katika Halmasahuri zaidi ya moja ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga (Shinyanga MC) na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Shinyanga DC).

Wilaya hiyo ina jumla ya walimu 2576 wanaofundisha shule za msingi na sekondari za Serikali. Katika Idadi hiyo walimu 917 ni wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga na walimu 1659 ni wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Kwa upande wa idadi ya shule za Serikali, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ina jumla ya shule 136 za msingi na 28 za sekondari pamoja na shule shikizi 4 huku Halmashauri ya Manispaa ikiwa na shule 148 za msingi na 18 za sekondari.

Katika ajira zilizotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan hivi karibuni, Wilaya ya Shinya ilipata walimu wapya 44 ambapo 34 walipangiwa Halmashauri ya Wilaya (Shinyanga Vijijini) na Walimu 10 walipangiwa Halmashauri ya Manispaa.

Happiness Mlangi ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC katika Wilaya ya Shinyanga na alipata fursa ya kufanya mahojiano na Jarida la Sauti ya TSC hivi karibuni ambapo alizungumzia masuala mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake katika kusimamia Ajira, Maadili na maendelo ya walimu wilayani hapo.

Akianza na zoezi la upandishaji wa madaraja/vyeo kwa walimu lililofanyika mwezi Juni 2021, Mlangi alieleza kuwa jumla ya walimu 1090 walipandishwa ambapo 545 ni wa Manispaa ya Shinganya na wengine 545 ni kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Hata hivyo, Mlangi alieleza kuwa walimu wanne hawakuweza kupandishwa vyeo kwa kuwa walikuwa wanakabiliwa na



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Shinyanga, Happiness Mlangi akiwa ofisini kwake.*



*Mkuu Idara ya Utawala na Rasilimali Watu katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Getrude Gisema akiwa pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali TSC, Gerard Chami (kulia) pamoja na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Shinyanga, Happiness Mlangi (kulia). Viongozi hao walikutana hivi karibuni ambapo walizungumzia masuala mbalimbali yanayohusu utumishi wa walimu katika Halmashauri hiyo.*

# TSC Shinyanga, Ofisi inayohudumia Halmashauri Mbili

mashauri ya nidhamu ambapo kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora hawakuwa na sifa za kupandishwa madaraja.

Alieleza kuwa kazi ya upandishaji vyeo walimu ilifanyika kwa ushirikiano mkubwa kati ya TSC na Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri zote mbili ambapo iliwalazimu kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha walimu wote waliopandishwa wanaingizwa kwenye mfumo ndani ya muda uliokuwa umetolewa.

"Zoezi la promotion (upandishaji wa madaraja) tulilifanya vizuri na kwa kweli tulikuwa tunakesha kuhakikisha walimu wetu tunawaingiza kwenye mfumo ndani ya muda uliokuwa umewekwa. Zoezi hilo halikuwa rahisi hata kidogo lakini tunamshukuru Mungu kwani tulilifanya na kulikamisha kwa wakati", alisema Mlangi.

Kutokana na juhudi hizo za kukamilisha zoezi la upandishaji madaraja walimu, Kaimu Katibu Msaidizi huyo alieleza kuwa watumishi wawili katika ofisi yake walitunukiwa vyeti vya pongezi na Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga.

"Mkurugenzi wa Manispaa alitutunuku vyeti kutokana na kazi kubwa tuliyoifanya baada ya kuona kuwa walimu wote tumewaingiza kwenye mfumo ndani ya muda uliotakiwa. Hata CWT pia walifurahishwa na kazi kubwa tuliyoifanya kwa walimu, nao walituita na kutupongeza," aliesema Mlangi.

Kuhusu suala la nidhamu kwa walimu wa wilaya hiyo, Mlangi alieleza kuwa mashauri ya nidhamu yamepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na elimu ambayo ofisi yake imekuwa ikitoa kwa walimu ili wasijiingize kwenye makosa na kujikuta wanachukuliwa hatua za kinidhamu.

"Kwa sasa tuna mashauri ya nidhamu matatu tu ambapo mawili yanatoka Manispaa na moja linatoka Halmashauri ya Wilaya. Kipindi cha nyuma tulikuwa tunapokea mashauri ya nidhamu saba kwa robo mwaka, hivyo tukiangalia tunaona kuna mabadiliko makubwa katika nidhamu kwa walimu wetu," alisema Mlangi.

Pamoja na mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake, Mlangi anabainisha changamoto kadhaa ambazo zinarudusha nyuma kasi ya utoaji wa huduma bora kwa walimu katika wilaya yake ikiwa ni pamoja na ofisi yake kuhudumia halmashauri mbili na kufanya walimu kuhudumiwa na waajiri wawili ndani ya ofisi moja ya TSC.

Anaeleza kuwa kila mwajiri anaweza kuwa na namna yake katika kuwahudumia walimu katika eneo lake, hiyo inasababisha walimu anaowasimamia wasipate huduma sawa pale waajiri hao wanapokuwa na mitazamo tofauti katika suala moja linalohusu walimu.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Shinyanga, Happiness Mlangi akionesha cheti cha pongezi alichopewa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga baada ya kukamilisha kwa ufanisi zoezi la upandishaji vyeo walimu.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali TSC, Gerard Chami (kulia) akizungumza na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Shinyanga, Happiness Mlangi wakati Mkuu huyo wa Kitengo alipotembelea ofisi za TSC shinyanga hivi karibuni.*

## TSC Shinyanga, Ofisi inayohudumia Halmashauri Mbili

"Mimi ningependa walimu ninaowasimamia wawe wanapata huduma kwa usawa. Lakini kama unavyojua binadamu tunatofautiana, kila mwajiri anaweza kuwa na mtazamo wake katika jambo flani. Sasa hii inasababisha wakati mwingine walimu wa halmashauri moja wajione hawapati huduma kama walimu wa halmashauri nyingine na wakati huo huo ofisi yangu ndiyo inayowajibika kushughulikia hoja na malalamiko yao," alisema.

Vile vile umbali wa ofisi ya TSC na eneo la Iselamaganzi zilipo ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ni kilometa 50 ambapo miundombinu ya barabara siyo mizuri na hakuna uhakika wa usafiri.

"Kutoka hapa mjini tulipo kwenda kule usafiri ni shida sana, yaani kuna basi moja la kwenda huko, na ikitokea umechelewa likaondoka huwezi kuondoka. Walimu wanapata adha kubwa pale wanapohitaji huduma za ofisi yetu na hata sisi tunashindwa kushiriki katika masuala ya kijamii yanayotokea kwa walimu wetu kutokana na changamoto ya usafiri," alisema Mlangi.

Kwa upande wa mamlaka ya kwanza ya nidhamu ambayo inaanzia shuleni, Mlangi alieleza kuwa Wakuu wa Shule bado hawajatimiza wajibu wao ipasavyo katika kushughulikia masuala ya nidadhu kwa walimu kitu ambacho kinachangia kulea makosa ya walimu.

"Wakati mwingine tunaletewa mashauri ambayo ukiyaangalia yapo kwenye mamlaka ya wakuu wa shule kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Tume ya utumishi wa Walimu. Mashauri ya aina hiyo tunayarudisha kwa wakuu wa shule ili wao wenyewe wachukue hatua stahiki," alisema.

Kaimu Katibu Msaidiazi huyo, alihitimisha kwa kusema kuwa ofisi yake ina mkakati wa kuendelea kutoa elimu zaidi kwa walimu katika masuala yote yanayohusu utumishi wao na pia watakaa na wakuu wa shule ili kuwakumbusha mamkala yao katika kudhibiti nidhamu ya walimu kwa mujibu wa sheria.



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Shinyanga wakiwa katika picha ya pamoja kati ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali TSC, Gerard Chami (wa kwanza kushoto) wakati Mkuu huyo wa Kitengo alipotembelea ofisi za TSC Shinyanga hivi karibuni.*

# TSC YATINGA 16 BORA SHIMIWI, SOKA



*Wachezaji wa timu ya soka ya TSC wakiwa katika picha ya pamoja wakijiandaa kuingia uwanjani kwenye mashindano ya SHIMIWI.*



*Wachezaji wa timu ya soka ya TSC wakiwa katika picha ya pamoja wakijiandaa kuingia uwanjani kwenye mashindano ya SHIMIWI.*

**Na Mwandishi Wetu.**

Timu ya Mpira wa Miguu wanaume ya TSC imefanikiwa kufuzu katika hatua ya makundi na kuingia kwenye hatua timu 16 bora katika mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yanayofanyia mkoani Morogoro.

TSC ilifanikiwa kufika nafasi hiyo baada ya pata ushindi wa 2-1 dhidi ya OSHA, sare ya 2-2 dhidi ya Ujenzi, sare ya 2-2 dhidi ya Ofisi ya Waziri Mkuu huku ikipoteza 2-1 dhidi ya Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto.

Hata hivyo, timu hiyo haikufanukiwa kutinga hatua ya robo fainali baada ya kupoteza mchezo wake dhidi ya timu kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI).



*Wachezaji wakiwa uwanjani kwenye mashindano ya SHIMIWI.*

# TSC YATINGA 16 BORA SHIMIWI, SOKA



*Wachezaji wa timu ya soka ya TSC wakihamasishana ili kufanya vizuri wakati wa mashindano ya SHIMIWI*



*Mashabiki wa timu ya soka ya TSC wakishangilia timu yao wakati wa mashindano ya SHIMIWI mkoani Morogoro.*



*Mashabiki wa timu ya soka ya TSC wakishangilia timu yao wakati wa mashindano ya SHIMIWI mkoani Morogoro.*



*Wachezaji wakiwa uwanjani kwenye mashindano ya SHIMIWI.*




**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz* **Tovuti:** *www.tsc.go.tz*

***Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania*** ***tumeyautumishiwawalimutanzania***